



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA



21 Disemba, 2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA CHA WAANDISHI WA HABARI ZA
MICHEZO TANZANIA (TASWA)**

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwatangazia wanachama na wadau Chama cha waandishi wa habari za michezo Tanzania (TASWA) kuwa, uchaguzi wa viongozi wa Chama hicho unatarajiwa kufanyika Tarehe 28 Januari, 2023, uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Fomu za kugombea nafasi tofauti katika uchaguzi huo zitatolewa katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam na kupatikana katika tovuti ya Baraza ambayo ni www.bmt.go.tz kuanzia tarehe 21/12/2022 hadi tarehe 23/1/2023.

Usaili wa nafasi hizo unatarajiwa kufanyika tarehe 27/1/2023 katika ukumbi wa uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na:

Nafasi	Ada
1. Mwenyekiti	} 50,000/=
2. Makamu Mwenyekiti	
3. Katibu Mkuu	
4. Katibu Mkuu Msaidizi	
5. Mweka Hazina	
6. Mweka Hazina Msaidizi	
Wajumbe 6 wa kamati tendaji	30,000/=

Sifa za wagombea

1. Awe Raia wa Tanzania
2. Awe hajawahi kukutwa na kosa lolote la jinai na kufungwa gerezani
3. Awe na elimu kuanzia stahhada kwa nafasi za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Katibu Msaidizi.
4. Nafasi zingine awe na elimu kuanzia ngazi ya cheti na kuendelea.
5. Awe mwanachama wa chama cha waandishi wa Habari za Michezo (TASWA)

Malipo ya fomu yafanyike katika akaunti ya Baraza, kwa kutumia mfumo mpya wa malipo Serikalini.

Ili kuweza kupata namba ya utambulisho wa malipo (**control number**) mgombea anashauriwa kupiga namba za simu 0735 414 043 au 0735 892 889 kwa maelekezo zaidi.

Aidha, risiti ya malipo iwasilishwe Baraza pamoja na fomu zilizojazwa kwa umakini na usahihi na kuambatanishwa na nakala za nyaraka zote kulingana na sifa mahususi zilizoainishwa katika katiba ya chama hiki.

Hivyo Baraza linatoa wito kwa yeyote mwenye sifa kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi huo na maendeleo ya michezo nchini.

Imetolewa Na:



Najaha Bakari

Kaimu Mkuu wa kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano